BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA TISA LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MBILI

Kikao cha Nne – Tarehe 03 Disemba, 2018.
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Vyama vya Ushirika Nam. 4 ya Mwaka 1986 na Kutunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar ya Mwaka 2018 ambayo inaweka utaratibu wa Uundaji na Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Maendeleo ya Wanawake, Habari na Utalii kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Vyama vya Ushirika Nam. 4 ya Mwaka 1986 na Kutunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar ya Mwaka 2018 ambayo inaweka utaratibu wa Uundaji na Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo.

II. MASWALI:

Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

111. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Kuna maeneo kama mji wa Chake Chake katika soko la Tibirinzi kunahitajika kujazwa mchanga kwenye mikoko ili kupata eneo la ardhi kutoka Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais mpaka eneo lilipojengwa jengo la Ofisi ya Mbunge, Tibirinzi. Kufanya hivyo itasaidia eneo hilo kuzalisha na pia kuongeza upana, ambapo baadae linaweza kuwekwa soko kubwa, maegesho ya magari na biashara nyengine kufanyika.

(a) Je, Serikali inaonaje sehemu hiyo kujazwa ili kupata eneo pana ambalo baadae Serikali inaweza kufanya matumizi mbali mbali inayoyataka.

(b) Je, Serikali inaonaje maeneo yaliyovamiwa na maji ya chumvi Tibirinzi kujazwa ili kuzuia bahari isiongeze eneo la maji na mmong'onyoko.

(c) Je, Serikali inaonaje eneo la Tibirinzi, barabara inayokwenda Wesha nayo ikaanza kujazwa ili kuzuia maji yasiendelee kuja barabarani.

Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

25. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (JIMBO la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Miezi michache iliyopita, Mheshimiwa Waziri na Serikali ya Mkoa walifanya ziara katika masoko ya Mjini Unguja ya Darajani, Mombasa na Mwanakwerekwe, hatua ambayo inastahili kupongezwa kwa ufuatiliaji wa kazi na kutatua changamoto.

(a) Je, ni mambo gani Mheshimiwa Waziri ameyabaini katika ziara hiyo.

(b) Je, hatua gani zinachukuliwa hivi sasa kutokana na yaliyobainika katika ziara hiyo.

(c) Je, maagizo yepi yameshatekelezwa mpaka hivi sasa kutokana na ziara hiyo.

83. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ:

Je, ni mitaro mingapi imechimbwa ambayo imekuwa korofi kwa wananchi na gharama gani SMZ zimetumika bila kutegemea fedha za wahisani.

<u>Wizara ya Fedha na Mipango</u>:

119. MHESHIMIWA SAID OMAR SAID (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:

Naipongeza Serikali kwa kujenga kiwanja cha kufurahishia watoto kisiwani Pemba katika Wilaya ya Chake Chake. Hata hivyo, inasemekana kwamba kiwanja hicho hakihudhuriwi na watu wengi hasa katika kipindi cha mwisho wa wiki. Kwa vile miongoni mwa sababu zinazoelezwa ni umbali uliopo kiwanja hicho kwa wananchi walioko maeneo ya Kaskazini Pemba hasa Wilaya ya Micheweni.

Je, Serikali haioni umuhimu wa kujenga kiwanja katika Wilaya ya Micheweni ili kuwapunguzia masafa wananchi na kukuza kipato katika maeneo yao.

Wizara ya Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

97. MHESHIMIWA SULEIMAN SARAHAN SAID (Jimbo la Chake Chake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo:

Katika michezo, imekuwa kawaida ulimwenguni kuwa na vilabu vya mpira ambavyo vinashindana kwa utajiri. Wasanii na wachezaji mmoja mmoja wa michezo na fani mbali mbali huwa wanalipwa na kujulikana pato lao.

(a) Je, ni "club" gani ya mpira wa miguu iliyo tajiri zaidi hapa Zanzibar na ina utajiri wa kiasi gani.

(b) Je, mchezaji gani wa mpira wa miguu aliye tajiri hapa Zanzibar na ana utajiri wa kiasi gani.

(c) Ningependa kujua wanamichezo wa fani zote mmoja mmoja kwa kila fani wanaoshiriki michezo yote ya kimataifa na utajiri wao.

Wizara ya Afya:

8. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa muda mrefu sasa paa la Hospitali ya Chake Chake limekuwa bovu na kuleta usumbufu kwa wagonjwa wanaolazwa hapo hasa mama wajawazito.

Je, kwanini muda mrefu paa hilo halifanyiwi matengenezo ya kudumu ili kuondosha usumbufu kwa wagonjwa na wafanyakazi.

Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

76. MHESHIMIWA SIMAI MOHAMMED SAID (Jimbo la Tunguu) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Je, ni kiasi gani cha fedha hadi sasa kimetolewa kwa vikundi vya Mkoa wa Kusini Wilaya ya Kati, Jimbo la Tunguu kupitia Mabaraza ya Vijana

Wizara ya Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

23. MHESHIMIWA SULEIMAN SARHAN SAID (Jimbo la Chake Chake - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ardhi, Nyumba, Maji na Nishati:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imejitahidi kustawisha nyumba za maendeleo zikiwemo nyumba za Madungu, Chake Chake Pemba kwa kuzitengeneza na kuwa kivutio kikubwa. Lakini bado kuna nyumba zilizobakia katika maeneno hayo ambazo mpaka leo hazijafanyiwa matengenezo.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuzitengeneza nyumba hizo kwa hivi sasa.

(b) Je, ni tatizo gani lililofanya nyumba zile zisiendelee kutengenezwa.

(c) Na kama kuna mpango wa kuziendeleza, Je, zinaanza lini kutengenezwa.

Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

48. MHESHIMIWA MWANTATU MBARAK KHAMIS (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi:

Kumekuwa na changamoto ya wizi wa mifugo na kupelekea wafugaji kukata tamaa na kuvunjika moyo na hali hiyo.

Je, Wizara ina mpango gani unaoutekelezeka ili kuona wananchi wanaendelea na kuimarisha shughuli zao za mifugo.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

88. MHESHIMIWA SHEHE HAMAD MATTAR (Jimbo la Mgogoni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Serikali yetu inachukuwa jitihada kubwa katika kuleta maendeleo kwa wananchi wake kwa kutekeleza Ilani ya CCM kwa asilimia kubwa. Lakini tunaona kwamba viwanja vyetu vya ndege bado vinakabiliana na changamoto nyingi.

(a) Je, ni lini Wizara itajenga sehemu ya kutosha kwa ajili ya kukaa wasafiri katika kiwanja cha ndege Pemba.

(b) Je, ni lini Wizara itaweka sehemu maalum ya kukaa wasafiri wa ndani (*Domestic*) ambao wamefika kiwanja cha Kimataifa cha A.A. Karume – Unguja ambao muda wao wa kufanya uhakiki (cheking) hau jafika badala ya sasa wanavyosumbuka.

32.. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Paje) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji:

Bandari ya Zanzibar imenunua krini mpya, lakini hivi sasa kumejitokeza tatizo la krini na kusababisha usumbufu kwa wafanya biashara kutopata mizigo yao kwa wakati ikiwemo mbatata, vitunguu, nafaka na hivyo Serikali kukosa mapato na kukaa meli ukutani ili kupisha meli nyengine.

(a) Je, Wizara inatoa kauli gani kuhusu suala la krini hasa kwa kuwa krini hiyo haifanyi kazi bure.

(b) Je, lini Shirika la Bandari litafanya maamuzi ya kununua vitendea kazi ili kuiwezesha Bandari kufanya kazi kwa wakati.

III. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Kazi, Uwezeshaji, Wazee, Wanawake na Watoto:

Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Vyama vya Ushirika Nam. 4 ya Mwaka 1986 na Kutunga Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar ya Mwaka 2018 ambayo inaweka utaratibu wa Uundaji na Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika na Mambo Mengine Yanayohusiana na Hayo - Kusomwa kwa Mara ya Pili.

Zanzibar,
03 Disemba, 2018.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA.